

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

WILAYA YA ILALA

Anwani ya Simu:

Simu: 022 – 2203185/2203182

Unapojibu Tafadhali taja:

Kumb. Na.CAB.32/235/01/51



1 BARABARA YA RASHIDI KAWAWA,
OFISI YA MKUU WILAYA YA ILALA,
S. L.P. 15486,

12881 DAR ES SALAAM

18 Julai, 2022


Yah: TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI WA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

Mkuu wa Wilaya ya Ilala anapenda kuwatangazia waombaji wa ajira ya muda za Sensa ya watu na makazi mwaka 2022, kwa nafasi ya **Karani wa Sensa na Wasimamizi wa Maudhui waliokidhi vigezo (Sifa)** kufika kwenye usaili utakaofanyika siku ya **Jumatano tarehe 20/07/2022** hadi Alhamisi tarehe **21/07/2022** katika **KATA** zao walizoomba kuanzia saa **1:00 asubuhi** isipokuwa **wasimamizi wa Tehama** ambao usaili wao utafanyika Ngazi ya **Halmashauri ya Jiji** katika **Ukumbi wa Shule ya Msingi Mnazimmoja** tarehe **20/07/2022** hadi **21/07/2022**.

WASAILIWA WANAPASWA KUZINGATIA YAFUATAYO;

1. Wasailiwa wote wanajulishwa kufika na vyeti vyote halisi (**Original Certificates**) vya kuanzia kidato IV na vyeti vya mafunzo ya ujuzi kulingana na nafasi aliyoomba na sio result slip, pamoja na **cheti halisi cha Kuzaliwa**.
2. Aidha atakayekuja na **“Transcript”** au **“Result Slip”** pekee bila vyeti halisi hataruhusiwa kufanya usaili.
3. Kila msailiwa atajigharamia kwa chakula, usafiri na malazi.
4. Wale ambao hawataona majina yao kwenye Tangazo hili watambue kwamba maombi yao hayakufanikiwa na wasisite kuomba tena mara nafasi nyingine zitapotangazwa. Orodha ya Waombaji waliokidhi vigezo imeambatanishwa hapa chini na kwenye tovuti ya Halmashauri ya Jiji

www.dcc.go.tz


Arch. Ng'wilabuzu N. Ludigija

**MWENYEKITI WA KAMATI YA SENSA WILAYA
WILAYA YA ILALA**

**MKUU WA WILAYA
WILAYA YA ILALA**